

That All May Be Edified

By Brother Chad H Webb

First Counselor in the Sunday School General Presidency

Ili Wote Waweze Kujengwa

Na Kaka Chad H. Webb

Mshauri wa Kwanza katika Urais Mkuu wa Shule ya Jumapili

October 2025 general conference

As we focus on Jesus Christ, teach His doctrine, and learn diligently, we invite the Holy Ghost to deepen our faith in Jesus Christ and help us become more like Him.

A story is told of a young university student who struggled with a challenging class, so he hired a tutor to help him. Near the end of the course, the professor announced that students could bring to the final exam one piece of paper on which they could place anything they wanted. Some students prepared by making tiny notes with information from lectures and textbooks, readable only by using a magnifying glass. But the young man arrived at the final exam with a blank sheet of paper and a stranger. When the professor questioned him, the young man replied, "You said I could bring one piece of paper with anything on it." He then placed the paper on the floor next to his desk and said, "I'd like my tutor to stand on my piece of paper."

The Holy Ghost

As members of The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, blessed with the companionship of a member of the Godhead, we can have the help of the perfect Tutor. The Holy Ghost knows all things, testifies of truth, and will "bring all things to [our] remembrance." President Russell M. Nelson frequently spoke about the importance of hearing the voice of the Lord. He taught us how to invite the guidance of the Holy Ghost and repeatedly pleaded with us to increase our spiritual capacity to receive revelation.

Tunapofokasi kwa Yesu Kristo, kufundisha mafundisho Yake na kujifunza kwa bidii, tunamkaribisha Roho Mtakatifu kuimarisha imani yetu katika Yesu Kristo na kutusaidia kuwa kama Yeye.

Hadithi inaelezea kuhusu mwanafunzi mdogo wa chuo kikuu ambaye alipambana na darasa lenye changamoto, hivyo alikodisha mkufunzi kumsaidia. Karibu na mwisho wa kozi, profesa alitangaza kwamba wanafunzi wanaweza kuleta kwenye mtihani wa mwisho karatasi moja ambayo wanaweza kuweka chochote wanachotaka. Wanafunzi wengine walijiandaa kwa kutengeneza vidokezo vidogo vya habari kutoka kwa mihadhara na vitabu vya masomo, vinavyosomwa tu kwa lenzi ya kukuza. Lakini kijana mdogo alifika kwenye mtihani wa mwisho akiwa na karatasi tupu na mgeni. Wakati profesa alipomuuliza, kijana mdogo alijibu "Ulisema ningeweza kuleta karatasi moja yenye chochote juu yake." Kisha akaweka karatasi chini karibu na meza yake na kusema, "Ningependa mkufunzi wangu asimame juu ya karatasi yangu."

Roho Mtakatifu

Kama waumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, tukiwa na baraka ya wenza wa mshiriki wa Uungu, tunaweza kupata msaada wa Mwalimu kamili. Roho Mtakatifu anajua mambo yote, anashuhudia ukweli, na ataleta mambo yote kwenye kumbukumbu [zetu]. Rais Russell M. Nelson alizungumza mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kuisikiliza sauti ya Bwana. Alitufundisha jinsi ya kualika ulinzi wa Roho Mtakatifu na alitusihi mara kwa mara sisi tuongeze uwezo wetu wa kiroho wa kupokea

Today I invite you to consider the role of the Holy Ghost, specifically related to gospel learning and teaching in the home and at church. The Holy Ghost is given by the prayer of faith and as we strive to live worthy of this precious gift. The inspired Church manual Teaching in the Savior's Way outlines additional principles the Lord has established that will help invite the influence of the Holy Ghost.

Invite Diligent Learning

One of these principles is to invite diligent learning. In the past, we may have thought of teaching as a chance for a parent or teacher to invite the Spirit into their own preparation and then share what they have learned with children or class members, whose role it has been to listen. But even more effective is when we, as learners, also come prepared and when teachers create learning experiences that foster personal revelation directly to our hearts and minds. Then, as we're given opportunities to share what we are learning through our study and from the Holy Ghost, we help each other to be instructed and edified. As we apply gospel principles, the Spirit again bears witness of their truthfulness.

As in all things, Jesus Christ is the perfect example. He has invited each of us to be diligent learners and to take charge of our own testimonies. He invited His disciples to prepare to learn, to share what they were learning, and to act in faith. He prayed for them, saw their divine potential, listened to them, and helped them know they were loved and needed.

As teachers, we can focus more on the learner's progress, on meeting their needs, and on helping them to develop spiritual habits of lifelong discipleship. As learners, when we exercise our agency in the learning process, we signal to the Holy Ghost our willingness to be taught by Him.

I'm grateful for a teacher who invited me to be a better learner. When I began college, I mistakenly thought of school as something to endure in order to be allowed to play sports. One day, after reading a paper I had written, my professor told me she thought I was a gifted analytical thinker. I didn't even know what that meant. She

ufunuo.

Leo nakualika utafakari jukumu la Roho Mtakatifu, hasa kuhusiana na kujifunza na kufundisha injili nyumbani na kanisani. Roho Mtakatifu hutolewa kwa sala ya imani na tunapojitahidi kuishi kwa kustahili kipawa hiki cha thamani. Kitabu cha Kiada cha Kanisa Kufundisha katika Njia ya Mwokozi kinabainisha kanuni za ziada ambazo Bwana amezianzisha ambazo zitasaidia kualika ushawishi wa Roho Mtakatifu.

Alika Kujifunza kwa Bidii

Moja ya kanuni hizi ni kualika kujifunza kwa bidii. Hapo zamani, tunaweza kuwa tulidhani kwamba kufundisha ni fursa kwa mzazi au mwalimu kumkaribisha Roho katika maandalizi yao wenyewe na kisha kushiriki kile walichojifunza na watoto au darasa, ambao jukumu lao lilikuwa kusikiliza. Lakini bora zaidi ni wakati sisi, kama wanafunzi, pia kujiandaa na pale walimu wanapotengeneza uzoefu wa kujifunza ambao unakidhi ufunuo binafsi moja kwa moja kwenye mioyo na akili zetu. Kisha, tunapopata fursa za kushiriki kile tunachojifunza kupitia masomo yetu na kutoka kwa Roho Mtakatifu-tunaweza kusaidiana kuelekezwa na kujengwa. Tunapokuwa tukitumia kanuni za injili, Roho tena atashuhudia ukweli wake.

Kama katika vitu vyote, Yesu Kristo ni mfano sahihi. Amemwalika kila mmoja wetu kuwa wanafunzi mwenye biddiina kushughulikia shuhuda zetu wenyewe. Aliwaalika wanafunzi Wake kujiandaa kujifunza, kushiriki yale waliyokuwa wanajifunza, na kutenda kwa imani. Aliomba kwa ajili yao, aliona uwezekano wao wa kiroho, aliwasikiliza, na kuwasaidia kujua kuwa walipendwa na kuhitajika.

Kama walimu, tunaweza kuzingatia zaidi maendeleo ya mwanafunzi, kukidhi mahitaji yao, na kuwasaidia kukuza tabia za kiroho za ufuasi wa maisha yote. Kama wanafunzi, tunapofanya kazi kwa uamuzi wetu katika mchakato wa kujifunza, tunamwonyesha Roho Mtakatifu kutaka kwetu kufundishwa Naye.

Nina shukuru kwa mwalimu ambaye alinialika niwe mwanafunzi bora. Nilipokuwa naanza chuo kikuu, nilifikiri vibaya kuhusu shule kama kitu cha kustahimili ili niweze kucheza michezo. Siku moja, baada ya kusoma insha niliyoandika, profesa wangu alinambia alidhani mimi ni mfikiriaji mzuri wa kiuchambuzi. Sikuwa na

said that with more focused effort, I could be a good student. That thought had never crossed my mind. Her interest, encouragement, and invitations changed the course of my education and greatly blessed my life.

Teach the Doctrine

Another principle relevant to inviting the Holy Ghost is to teach true doctrine. This means that our gospel study and instruction are rooted in the word of God and that we don't sensationalize or speculate on what the Lord has not revealed. Instead, we focus on essential and eternal gospel principles, which allows the Spirit to testify of truth. Again, we follow the example of the Savior. He said, "My doctrine is not mine, but his that sent me."

True doctrine is found in the scriptures and teachings of modern prophets. The Lord's exhortation to study the scriptures individually and as families and to attend church each week to study His gospel provides a remarkable framework to learn His doctrine and hear His voice. We search the scriptures to understand the narrative, the principles they teach, and the application of these truths in our lives. What a blessing it is to have the scriptures at our fingertips. Imagine Adam and Eve, Abinadi, or even the Master Teacher, Jesus Christ, visiting our homes or classes to teach us. They can when we feast upon the word of God. With consistent effort, we can learn to understand and love the scriptures and trust that they have the answers to the questions of the soul.

There was a time before we were married when my wife, Kristi, was struggling to feel Heavenly Father's love and to understand His plan for her. As she prayed for guidance, an impression came that she should attend institute, so she enrolled in a New Testament class. The way her institute teacher taught from the scriptures, even the way he held them, showed how much he loved the word of God. As she attended, the Holy Ghost whispered to her that there was something in the scriptures that she needed. Her teacher's love for the scriptures and the promptings of the Holy Ghost gave her a desire to begin a serious study of the word of God—which became a life-

hata ufahamu wa maana yake. Alisema kwamba kwa juhudi zaidi zenye mtazamo uliozingatiwa, naweza kuwa mwanafunzi mzuri. Wazo hilo lilikuwa halijawahi kupita akilini mwangu. Hamu yake, himizo na mwaliko vilibadilisha mkondo wa elimu yangu na kuja kunibariki sana katika maisha yangu.

Fundisha Mafundisho

Kanuni nyingine sambamba na kumwalika Roho Mtakatifu ni kufundisha mafundisho ya kweli. Hii ina maana kwamba mafunzo yetu ya injili na maelekezo vina msingi katika neno la Mungu na kwamba hatufanyi mambo kuwa makubwa au kubashiri kuhusu kile ambacho Bwana hajadhihirisha. Badala yake, tunazingatia kanuni muhimu na za milele za injili, ambazo zinamwezesha Roho kutoa ushuhuda wa ukweli. Tena, tunafuata mfano wa Mwokozi. Alisema, "Mafunzo yangu si yangu mimi, ila ni yake yeye aliyenipeleka."

Mafundisho ya kweli yanapatikana katika maandiko na katika mafundisho ya manabii wa siku hizi. Mwaliko wa Bwana wa kujifunza maandiko binafsi kama familia kuhudhuria kani-sanikila wiki kujifunza injili. Yake unatoa mfumo mzuri wa kujifunza mafundisho. Yake na kuisikia sauti Yake. Tunapekua maandiko ili kuelewa simulizi, kanuni wanazofundisha na matumizi ya kweli hizi katika maisha yetu. Ni baraka kubwa kiasi gani kuwa na maandiko mikononi mwetu. Fikiria Adamu na Hawa, Abinadi, au hata Mwalimu Mkuu Yesu Kristo wakitembelea nyumba zetu au madarasa yetu ili kutufundisha. Wanaweza kama tunasherehekea neno la Mungu. Kwa juhudi endelevu, tunaweza kujifunza kuelewa na kupenda maandiko na kuamini kwamba yana majibu ya maswali ya nafsi.

Kulikuwa na wakati kabla ya kuoana kwetu ambapo mke wangu Kristi, alikuwa anasumbuka kuhisi upendo wa Baba wa Mbinguni na kuelewa mpango Wake kwa ajili yake. Alipokuwa akiomba mwongozo, wazo lilikuwa kwamba anapaswa kuhudhuria chuo (institute), hivyo alijiandikisha katika darasa la Agano Jipya. Jinsi mwalimu wake wa darasa hilo alivyofundisha kutoka kwenye maandiko, hata jinsi alivyoshika maandiko hayo, ilionyesha jinsi alivyolipenda neno la Mungu. Alipohudhuria, Roho Mtakatifu alimnong'oneza kwamba kulikuwa na kitu katika maandiko ambacho alikihitaji. Upendo wa mwalimu wake kwa maandiko na mwongozo wa Roho Mtakatifu

long journey of deep conversion and consecrated service.

Focus on Jesus Christ

Finally, as Teaching in the Savior's Ways suggests, our teaching and learning should always focus on Jesus Christ. We can speak more often and more reverently of Him and seek more opportunities to express testimony, gratitude, and love for Him. Whatever the setting, as we remember Him, we can have "his Spirit to be with [us]."

One way to place Jesus Christ at the center of our teaching is to emphasize that He is the perfect example, the embodiment and expression of all gospel principles. Even when He is not directly referred to in a scriptural account, we can still point to Him as the example of the principle being taught. We might simply ask, "Can you think of a time when Jesus Christ exemplified this principle?"

We can also focus on Him by learning of His titles, roles, and attributes, seeking not only to learn what He has done but also to better understand who He is. For example, when studying the principle of repentance, it's important to understand how to repent. But it's also essential to remember what Jesus Christ has done to make repentance possible and to understand what repentance teaches us about Him, about His true nature and characteristics. What does our opportunity to repent say about His love, patience, and mercy, His belief in our divine potential, His willingness to atone for our sins, and the joy He finds in forgiving? And understanding His titles—such as Lamb of God, Redeemer, and Physician—helps us see that repentance is His invitation to cleanse, change, and heal us. Focusing on what He has done for us and what it says about who He is can help us have "faith unto repentance."

At times, we may not immediately see the attributes of the Savior outlined in a scriptural account. For example, when reading about Nephi building a boat, we might focus only on Nephi. But focusing on the Savior can help us see that this record was not preserved to teach us about the greatness of Nephi but to show us the greatness of God—that He gives us strength to keep

vilimpa tamanio la kuanza kujifunza kwa makini neno la Mungu—ambalo lilikuwa safari ya maisha ya uongofu wa kina na huduma iliyowekwa wakfu.

Fokasi kwa Yesu Kristo

Hatimaye, kama Kufundisha katika Njia ya Mwokozi inavyopendekeza, kufundisha na kujifunza kwetu lazima kufokasi kwa Yesu Kristo. Tunaweza kuzungumza zaidi mara kwa mara na kwa heshima zaidi kuhusu Yeye na kutafuta nafasi zaidi za kutoa ushuhuda, shukrani na upendo Kwake. Iwe katika mazingira yoyote, tunapomkumbuka, tunaweza kuwa na "Roho wake awe pamoja [nasi]"

Njia moja ya kumweka Yesu Kristo katikati ya mafundisho yetu ni kuonyesha kwamba Yeye ndiye mfano mkamilifu, halisi na dhihirisho la kanuni zote za injili. Hata pale ambapo Hajatajwa moja kwa moja katika simulizi ya maandiko, bado tunaweza kumuona kama kielelezo cha kanuni inayofundishwa. Tunaweza kuuliza kwa urahisi, "Je, unaweza kukumbuka wakati ambao Yesu Kristo alikuwa mfano wa kanuni hii?"

Tunaweza pia kufokasi Kwake kwa kujifunza majina, majukumu, na sifa Zake, kujifunza si tu kuhusu kile alichofanya bali kuelewa vyema kuhusu Yeye ni nani. Kwa mfano, tunapojifunza kanuni ya toba, ni muhimu kuelewa jinsi ya kutubu. Lakini pia ni muhimu kukumbuka kile Yesu Kristo alichokifanya kuwezesha toba na kuelewa kile toba inachotufundisha kumhusu Yeye, kuhusu asili Yake ya kweli na tabia Zake. Fursa yetu ya kutubu inasema nini kuhusu upendo Wake, uvumilivu na rehema, imani Yake katika uwezo wetu wa kimungu, utayari Wake wa kulipia dhambi zetu na furaha anayoipata katika kusamehe? Na kuelewa majina Yake—kama vile Mwanakondoo wa Mungu, Mkombozi na Tabibu—kunatusaidia kuona kwamba toba ni mwaliiko Wake wa kusafisha, kubadilisha na kutupony. Kufokasia yale ambayo ameyafanya kwetu na yale yasemwayo kuhusu Yeye yanaweza kutusaidia kuwa na "imani iongozayo kwenye toba."

Wakati fulani, tunaweza tusione kwa haraka tabia za Mwokozi zilizoelezwa kwenye hadithi za maandiko. Kwa mfano, tunaposoma kuhusu Nefi akijenga mashua, tunaweza kumfokasia zaidi Nefi. Lakini kumfokasia Mwokozi tunaweza kutusaidia kuona kwamba rekodi hii haikuhi-fadhiwa kutufundisha kuhusu ukuu wa Nefi bali kutuonyesha ukuu wa Mungu—kwamba Anatu-

His commandments and delivers us in times of need.

We can also focus on Jesus Christ's central role in Heavenly Father's perfect plan of happiness. It can change the course of our lives to see our circumstances through the lens of God's eternal plan instead of seeing the plan through the lens of our temporal circumstances. The gospel is not a list of demands; it's the good news that Jesus Christ overcame sin and death. It is by accessing His amazing grace through keeping our covenants with God that we can live joyfully now and prepare for life with our Father in Heaven in the eternities. As we learn to see Heavenly Father and the Savior in the scriptures, we will come to know Them better and we will see Their love and influence more frequently and more powerfully in our own lives.

I will always remember the Spirit I felt as a youth when our teacher taught about the final days of the Savior's life. He helped us see the significance of the events in the upper room, Gethsemane, Golgotha, and the empty tomb. He shared his profound gratitude for the Savior and his consuming desire to follow Him. His teaching was an invitation for the Holy Ghost to testify of Jesus Christ. And the Spirit I felt in that class deepened my faith and increased my love and appreciation for the Savior. The influence of that teacher has stayed with me my entire life. As was said of another teacher, "We could warm our hands by the fire of his faith."

Conclusion

In our homes and Church meetings, as we focus on Jesus Christ, teach His doctrine, and learn diligently, we invite the Holy Ghost to deepen our faith in Jesus Christ and help us become more like Him, which is the aim of all gospel teaching and learning.

I'm grateful for the teachers in my life, from goodly parents and local leaders and teachers to the men and women who have been called to teach and testify from this pulpit, who help us to know and follow Jesus Christ. And I'm grateful for the Holy Ghost, the perfect Tutor. It is through the Holy Ghost that I know that Heavenly Father loves us and has a perfect plan for us;

pa nguvu za kuzishika amri Zakena kutuokoa katika nyakati za shida.

Tunaweza pia kufokasia jukumu kuu la Yesu Kristo katika mpango mkamilifu wa furaha wa Baba wa Mbinguni. Inaweza kubadili mwelekeo wa maisha yetu kuona hali zetu kupitia lenzi ya mpango wa milele wa Mungu badala ya kuona mpango huo kupitia lenzi ya hali zetu za muda. Injili si orodha ya mahitaji; ni habari njema kwamba Yesu Kristo alishinda dhambi na kifo. Ni kwa kufikia neema Yake ya ajabu kwa kutunza maagano yetu na Mungu ndipo tunaweza kuishi kwa furaha sasa na kujiandaa kwa maisha pamoja na Baba yetu Mbinguni katika umilele. Tunapojifunza kumuona Baba wa Mbinguni na Mwokozi katika maandiko, tutakuja kuwaelewa vizuri zaidi na tutayaona mapenzi Yao na ushawishi wao mara nyingi na kwa nguvu zaidi katika maisha yetu.

Daima nitamkumbuka Roho niliyemhisi nikiwa kijana wakati mwalimu wetu alipofundisha kuhusu siku za mwisho za maisha ya Mwokozi. Alitusaidia kuona umuhimu wa matukio katika chumba cha juu, Gethsemane, Golgotha na kaburi lililokuwa tupu. Alishiriki shukurani zake za dhati kwa Mwokozi na tamani lake kubwa la kumfuata. Mafundisho yake yalikuwa mwali kwa Roho Mtakatifu kushuhudia kuhusu Yesu Kristo. Roho niliyoihisi katika darasa hilo aliongeza kina cha imani yangu na kuongeza upendo na shukurani zangu kwa Mwokozi. Ushawishi wa mwalimu huyo umebaki nami maisha yangu yote. Kama ilivyosemwa kuhusu mwalimu mwingine, "Tungeweza kupasha mikono yetu moto kwa imani yake."

Hitimisho

Katika mikutano nyumbani na Kanisani, tunapofokasi kwa Yesu Kristo, kufundisha mafundisho Yake na kujifunza kwa bidii, tunamkaribisha Roho Mtakatifu kuimarisha imani yetu katika Yesu Kristo na kutusaidia kuwa kama Yeye, ambalo ndilo lengo la kufundisha na kujifunza injili.

Nina shukurani kwa walimu katika maisha yangu, kutoka kwa wazazi wema na viongozi wa eneo husika na walimu hadi kwa wanaume na wanawake ambao wameitwa kufundisha na kushuhudia kutoka kwenye mimbari hii, wanaotusaidia kumjua na kumfuata Yesu Kristo. Na ninashukuru kwa Roho Mtakatifu, mwalimu mzuri. Ni kupitia Roho Mtakatifu ambapo najua

that Jesus is the Christ, the Savior and Redeemer of the world; and that His gospel and Church have been restored. I gratefully testify of these things in the name of Jesus Christ, amen.

kwamba Baba wa Mbinguni anatupenda na anao mpango mkamilifu kwa ajili yetu; kwamba Yesu ni Kristo, Mwokozi na Mkombozi wa dunia, na kwamba injili na Kanisa Lake vimerejeshwa. Nashuhudia kwa shukrani kuhusu mambo haya katika jina la Yesu Kristo, amina.